**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**

**MKATABA WA UFUNDI UMEME**
**JENGO LA KIBANDA CHA MLINZI**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 14 mwezi 01 2022

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha Mkoa wa Lindi, S.L.P. 1001, Lindi ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

HUMPHREY NGULUKO MADIWA S.L.P. 51, RUANGWA
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mafia;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mafia;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya UMEME HATUA YA UMAHIZIAJI

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA YA UFUNDI**
   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 100,000/=, sema; LAKI MOJA TU
   Fundi atafanya kazi ya UMEME HATUA YA UMAHIZIAJI
   kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.